**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA AROBAINI NA MOJA

**05 JUNI, 2017**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

### KIKAO CHA AROBAINI NA MOJA – TAREHE 05 JUNI, 2017

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la kudharau Mamlaka ya Spika linalowahusu Mheshimiwa Esther Amos Bulaya (Mb) na Mheshimiwa Halima James Mdee (Mb).

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**331. MHESHIMIWA MARYAM SALUM MSABAHA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Wafanyakazi wa Kampuni mbalimbali nchini wamekuwa wakipata ajali wawapo kazini na baadhi yao kutopewa huduma ya matibabu na

Waajiri wao na kuishia kupata ulemavu wa kudumu:-

Je, ni Wafanyakazi wangapi wamepata stahiki zao baada ya ajali.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**332. MHESHIMIWA MAULID SAID MTULIA (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Sera yetu ya Afya ni kuchangia gharama ili kupata huduma ya afya isipokuwa kwa Wazee, Mama na Mtoto:-

Je, ni fedha kiasi gani zimekusanywa kutokana na tozo za uchangiaji gharama za matibabu ndani ya miaka mitano (5) na ni nini matumizi ya fedha hizo.

**333. MHESHIMIWA MARTHA JACHI UMBULLA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Vifo vya akina Mama na Watoto kwa takwimu za hivi karibuni Mkoani Manyara vinatisha:-

Je, Serikali inatoa kauli gani ya mwisho ili kukabiliana na janga hili ikiwepo kuimarisha Vituo vyote vya huduma ya Mama na Mtoto vijijini bila kujali uwezo wa Wanawake kulipia au kutolipia huduma hiyo.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

### 334. MHESHIMIWA MARY DEO MURO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Mbuga ya Saadani iliyoko Mkoa wa Pwani ili kuongeza pato kwa Wananchi walio kando ya Mbuga hiyo.

### 335. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Kisiwa cha Mafia kina vivutio vingi vya utalii kama viumbe wanaoishi kwenye maji, mikoko nk. Lakini vivutio hivyo havijatangazwa vya kutosha:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutangaza utalii wa Kisiwa cha Mafia.

## WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

**336. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Kwa muda mrefu miembe imeendelea kushambuliwa na inzi na kuoza, minazi nayo hushambuliwa na ugonjwa wa kukauka na migomba hushambuliwa na ugonjwa wa mnyauko:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondokana na magonjwa hayo ili Wananchi wazidi kufaidika na matunda ya mazao yao.

## WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

**337. MHESHIMIWA HASSAN ELIAS MASALA (NACHINGWEA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Huko Nachingwea kulikuwa na viwanda viwili vya kukamua Ufuta na Korosho ambavyo vimebinafsishwa kwa muda mrefu lakini Wawekezaji hawajaviendeleza hadi sasa hivyo kupunguza ajira na mzunguko wa fedha:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani juu ya Wawekezaji waliopewa viwanda hivyo viwili;

(b) Kama Wawekezaji hao wameshindwa kuendeleza viwanda hivyo; Je, Serikali ina mpango gani na viwanda hivyo hasa ikizingatiwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imeonyesha nia ya kufufua viwanda nchini.

**338. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Tanzania imejaliwa kuwa na Almasi na Madini ya aina mbalimbali kwa wingi ikiwemo *Gypsum:-*

(a) Je, ni busara kwa viwanda vyetu humu nchini kuagiza *Gypsum* toka nje ya nchi;

(b) Je, Serikali haioni kuwa huo ni ubadhilifu na matumizi mabaya ya fedha za Watanzania;

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani kukomesha utaratibu huo ili kutunza fedha zetu chache za kigeni na kulazimisha ajira kwa Watanzania katika machimbo ya *Gypsum* hususan Itigi.

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**339. MHESHIMIWA DKT. RASHID MOHAMMED CHUACHUA (MASASI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi zinazopoteza fedha nyingi kwa ajili ya misamaha ya Kodi ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki kwa kigezo cha kuvutia wawekezaji; na katika Hotuba ya Bajeti 2013/2014 ya aliyekuwa Waziri wa Fedha, Marehemu Mhe. Dkt. William Mgimwa alisema misamaha ya Kodi kwa mwaka 2011/2012 ilifikia 4.3% ya Pato la Taifa:-

(a) Je, hali ya misamaha ya Kodi ikoje kwa sasa ikilinganishwa na ile ya mwaka 2011/2012;

(b) Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2009/2010 Tanzania ingepoteza asilimia 15 ya pato lililotarajiwa kukusanywa iwapo misamaha isingetolewa, 2010/2011 asilimia 8 na kwa mwaka 2011/2012 asilimia 27; Je, hali ya misamaha ya Kodi ikoje kuanzia 2013/2014 hadi sasa.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**340. MHESHIMIWA PHILIPO AUGUSTINO MULUGO (SONGWE)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mji wa Mkwajuni ndio Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Songwe. Katika Mji huo hakuna maji na idadi ya Wananchi na Wakazi wanaongezeka kwa kasi:-

Je, ni lini Serikali itajenga miradi ya maji katika Mji huo pamoja na sehemu nyingine zisizo na maji katika Jimbo la Songwe.

**IV. HOJA ZA KAMATI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la kudharau Mamlaka ya Spika linalowahusu Mheshimiwa Esther Amos Bulaya (Mb) na Mheshimiwa Halima James Mdee (Mb).

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**05 JUNI, 2017** **KATIBU WA BUNGE**